**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI**

# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

**MHESHIMIWA RAHMA KASSIM ALI (MBM)**

## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**MEI, 2025**

# UONGOZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI ZANZIBAR



**Mhe. Rahma Kassim Ali (MBM)**
**Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi**



Mhe. Salha Mhammed Mwinjuma
Naibu Waziri wa Ardhi na
Maendeleo ya Makaazi



Ndg. Khadija Khamis Rajab
Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na
Maendeleo ya Makaazi



Ndg. Mhaza Gharib Juma
Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi
na Maendeleo ya Makaazi



Ndg. Bakari Ali Bakari
Afisa Mdhamini



Ndg.Khamisuu H. Moh'd
Mkurugenzi Uendeshaji
na Utumishi



Ndg. Makame Salum Ali
Mkurugenzi Mipango
Sera na Utafiti



Ndg. Hannat H. Bakar
Mkurugenzi Maendeleo
ya Makaazi



Ndg. Mussa Kombo Bakar
Katibu Mtendaji
Kamisherni Ardhi



Ndg. Sultan Said Suleiman
Mkurugenzi Mkuu
Shirika la Nyumba



Ndg. Is-haka A. Khamis
Mwenyekti
Mahkama ya Ardhi



FRV. Tahir M. Omar
Mthamini Mkuu
wa Serikali

## YALIYOMO


UTANGULIZI ....................................................................................1
MUUNDO WA WIZARA..........................................................................4
MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO
YA MAKAAZI........................................................................................4
MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA
PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ................5
MUHTASARI WA MAPATO ..........................................................5
MUHTASARI WA MATUMIZI .......................................................6
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA
WA FEDHA 2024/2025 NA MWELEKEO KWA MWAKA
WA FEDHA 2025/2026. .....................................................................7
PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU
WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI ....8
PROGRAMU NDOGO SN020101: URATIBU WA
MIPANGO, SERA NA UTAFITI; ...................................................9
PROGRAMU NDOGO SN020102: UTAWALA NA UENDESHAJI..14
PROGRAMU NDOGO SN020103: URATIBU WA SHUGHULI
ZA WIZARA PEMBA. ........................................................................18
PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI ...............22
PROGRAMU NDOGO SN020201: USIMAMIZI WA ARDHI .....23
HN02020108: UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI................24
HN02020107: KUSIMAMIA NA KUIDHINISHA RIPOTI
ZA UTHAMINI ....................................................................................27
HN02020101: UPANGAJI NA USIMAMIZI WA ARDHI .............30
PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI ......37

PROGRAMU NDOGO SN020301: MAENDELEO YA MAKAAZI....................................................................38
HUDUMA HN02030102: USAJILI WA MAJENGO NA JUMUIYA YA KONDOMINIO....................................................38
HN02030105 UTATUZI WA MIGOGORO KWA WAPANGAJI WA NYUMBA.........................................................................42
SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR...........................................44
VIPAUMBELE VYA BAJETI YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026. ..............49
MAOMBI YA IDHINI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026. ..........................50
SHUKRANI..................................................................................51
HITIMISHO.................................................................................54
VIAMBATANISHO......................................................................55

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI MHESHIMIWA RAHMA KASSIM ALI (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR.**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika;** kwa ruhusa yako, naomba kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

2. **Mheshimiwa Spika;** Naanza Hotuba yangu kwa kumshukuru Allah (S.W) kwa kuendelea kutupatia neema yake ya uhai na uzima tukaweza kuhudhuria katika kikao cha kujadili Hotuba ya Wizara hii. Naendelea pia kumshukuru Allah kwa kutupatia uwezo na nguvu za kutekeleza majukumu tuliyojipangia.

3. **Mheshimiwa Spika;** kwa niaba ya Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoiongoza na kuleta Maendeleo endelevu ya Nchi yetu. Pia, amekuwa ni mfano mzuri katika kuimarisha Amani na Utulivu Nchini pamoja na usimamizi mzuri wa utekelezaji wa Mipango ya Kitaifa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025. Vilevile, ni muumini mzuri wa kuimarisha falsafa ya

Mashirikiano Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kumlinda pamoja na kumsimamia katika kutekeleza majukumu yake na nawaomba Wananchi wa Tanzania waendelee kumuamini na kumpa ridhaa ya kuendelea kuingoza Nchi yetu ili aendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

4. **Mheshimiwa Spika;** Kipekee, nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiongoza Zanzibar kwa kuzingatia misingi ya umoja, mshikamano, amani, utulivu pamoja na namna anavyosimamia kwa umakini mkubwa utekelezaji wa Mipango ya Kitaifa, Kikanda na Kimatifa hususan katika uendelezaji wa Sekta ya Ardhi na Makaazi. Pia, namshukuru kwa miongozo, maelekezo na ushirikiano wake anaotupatia katika kutekeleza majukumu aliyotukabidhi. Sote ni mashuhuda kwa namna anavyoipambania Zanzibar kuwa na Maendeleo endelevu kwa kuimarisha Sekta za kiuchumi, Kisiasa na Huduma za jamii ikiwemo Makaazi.

5. **Mheshimiwa Spika;** hivi karibuni tutaingia katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, kutokana na nia njema na maendeleo makubwa aliyoyaleta Rais wetu nawaomba Wazanzibari waendelee kumuamini kwani “Yajayo ni Neema Zaidi”. Pia, Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu, afya, hekima, busara na ustahamilivu katika kuingoza Zanzibar pamoja na kumuwezesha kufikia azma yake ya kuiletea Maendeleo makubwa.

6. **Mheshimiwa Spika;** Napenda kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamo wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamo wa Pili wa Rais kwa namna wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar pamoja na kusimamia na kufuatilia shughuli na miradi mbali mbali ya Serikali. Allah (S.W) azidi kuwapa nguvu, busara, hekima na afya njema ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

7. **Mheshimiwa Spika;** kwa namna ya pekee, napenda kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti kwa namna mnavyoliongoza Baraza kwa busara, hekima na uadilifu mkubwa. Vilevile nawashukuru wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa michango, ushauri, busara, hekima na Miongozo waliokuwa wakitupatia ambayo iliimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ufanisi.

8. **Mheshimiwa Spika;** Pia, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Yahya Rashid Abdalla, Makamo Mwenyekiti Mheshimiwa Aza Januar Joseph, Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati kwa mashirikiano makubwa waliyotupatia kwa kipindi chote tulichokua tukifanya kazi pamoja. Tunaahidi kwamba ushauri na maelekezo mliyotupatia tutaendelea kuyafanyia kazi katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, tunazishukuru Kamati zote za Baraza zilizofanya kazi na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.

## MUUNDO WA WIZARA

9. **Mheshimiwa Spika;** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imeundwa na Sekta ya Ardhi na Sekta ya Makaazi inayojumuisha Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango Sera na Utafiti, Idara ya Maendeleo ya Makaazi, pamoja na Ofisi Kuu Pemba. Aidha, Wizara ina Taasisi tatu (03) na Shirika moja ambazo ni Kamisheni ya Ardhi (COLA), Mahakama ya Ardhi, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali pamoja na Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC). Vilevile, Wizara ina Bodi Tendaji moja ambayo ni Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba.

## MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

10. **Mheshimiwa Spika;** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inatekeleza majukumu makuu yafuatayo:-

    1. Kutunga na kusimamia utekelezaji wa Sera za Kisekta na Sheria zinazohusiana na Ardhi, Nyumba na Makaazi;

    2. Kushajihisha na kutekeleza upatikanaji wa makaazi bora na nafuu kwa Wananchi;

    3. Kusimamia utambuzi, usajili, umiliki wa ardhi na shughuli za ujenzi Nchini;

    4. Kufanya tafiti zinazohusiana na Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi;

5. Kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi Nchini Mijini na Vijijini;

6. Kusimamia Rasilimali watu, fedha na Rasilimali nyenginezo za Wizara.

11. **Mheshimiwa Spika;** baada ya utangulizi huo, naomba sasa uniruhusu kuelezea utekelezaji wa Kazi za Kawaida na Maendeleo za Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Muelekeo wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### MUHTASARI WA MAPATO

12. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 4,270,000,000** kutoka vyanzo vyake vya Mapato vilivyomo ndani ya Fungu la Wizara (Ada ya Mahakama, Usajili wa Kondominio, Vibali vya Ujenzi na Ada ya Uthamini) ambapo **TZS Bilioni 3,202,500,000** ilikadiriwa kukusanywa kwa kipindi cha Miezi Tisa. Vilevile, Wizara kupitia Kamisheni ya Ardhi ilikadiriwa kukusanya **TZS Bilioni 6,224,320,746** kwa ajili ya Mapato yanayotokana na Nyaraka za Ardhi, Muongozo wa Matumizi ya Ardhi, Upimaji na Ramani, Usajili wa Ardhi, Uhaulishaji na Ada ya Uthamini, kati ya hizo **TZS Bilioni 4,668,202,512** ilikadiriwa kukusanywa kwa kipindi cha Miezi Tisa.

13. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **TZS Bilioni 1,633,793,271** zimekusanywa sawa na **asilimia 51** ya makadirio ya makusanyo ya Miezi Tisa na **asilimia 38** ya makadirio ya Mwaka. Kiambatanisho nambari 1 (a) kinafafanua. Aidha, kwa upande wa Kamisheni ya Ardhi hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **TZS Bilioni 5,435,353,178** zimekusanywa sawa na **asilimia 116** ya makadirio ya makusanyo ya Miezi Tisa na **asilimia 87** ya makadirio ya Mwaka.

## MUHTASARI WA MATUMIZI

14. **Mheshimiwa Spika;** kwa upande wa matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ilipangiwa kutumia Jumla ya **TZS Bilioni 53,062,900,000**, kati ya hizo **TZS Bilioni 5,014,600,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Kazi za Kawaida kwa fungu la Wizara, ambapo kati ya fedha hizo jumla ya **TZS Bilioni 2,613,100,000** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara kwa Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Bilioni 2,085,100,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya uendeshaji wa Ofisi kwa Idara zilizo chini ya Wizara na **TZS Milioni 316,400,000** ni Ruzuku kwa ajili ya Taasisi za Wizara, **TZS Bilioni 3,003,300,000** zilitengwa kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara ya Kamisheni ya Ardhi, **TZS Billioni 45,000,000,0000** kwa Kazi za Maendeleo na asilimia **50** ya makusanyo kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Kamisheni ya Ardhi.

15. **Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Makadirio ya Miezi Tisa Jumla ya **TZS Bilioni 39,841,209,440** ziliidhinishwa

(**TZS Bilioni 3,716,925,940** ni utekelezaji wa kazi za kawaida, ambapo kati ya fedha hizo **TZS Bilioni 1,959,825,210** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara kwa Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Bilioni 1,757,100,730** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya uendeshaji wa Ofisi kwa Idara zilizo chini ya Wizara na **TZS Milioni 272,590,000** ni Ruzuku kwa ajili ya Taasisi za Wizara, **TZS Bilioni 2,101,693,500** zilitengwa kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara ya Kamisheni ya Ardhi, **TZS Billioni 33,750,000,0000** kwa kazi za Maendeleo na **asilimia 50** ya makusanyo kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Kamisheni ya Ardhi.

16. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **TZS Bilioni 27,520,856,586.75** zimepatikana sawa na **asilimia 73** kwa makadiro ya Miezi Tisa na **asilimia 55** kwa makadirio ya mwaka ambapo **TZS Milioni 624,373,667** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (OC), **TZS Bilioni 1,854,265,299** kwa ajili ya Mishahara, **TZS Milioni 112,590,000** kwa ajili ya Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida, **TZS Bilioni 2,270,555,233** kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara na **TZS Bilioni 22,659,099,588** kwa ajili ya Kazi za Maendeleo. **Kiambatanisho nambari 1 (b) kinafafanua.**

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA MWELEKEO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

17. **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara imetekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu

tatu ambazo ni **Programu PN0201:** Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, **Programu PN0202:** Usimamizi wa Ardhi na **Programu PN0203**: Maendeleo ya Makaazi.

## PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

**18.** **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu PN0201 ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ina jukumu la kuimarisha uratibu katika utekelezaji wa kazi za Wizara ambayo inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo n**i Programu ndogo SN020101** ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti; **Programu Ndogo SN020102** ya Uendeshaji na Utumishi na **Programu Ndogo ya SN020103** ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

**19.** **Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, **Programu Kuu PN0201** ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 2,170,000,000** kutokana na vyanzo vyake vya Mapato na **TZS Bilioni 1,627,500,000** ilikadiria kukusanywa kwa Miezi Tisa.

**20.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, fedha zilizokusanywa ni **TZS Milioni 386,829,100** sawa na **asilimia 24** kwa Miezi Tisa na asilimia **19** kwa Mwaka.

**21.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Kuu PN0201 ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 8,522,969,000 (TZS Bilioni 2,072,869,000**

Mishahara, **TZS Bilioni 1,450,100,000** Matumizi ya Kawaida na **TZS Bilioni 5,000,000,000** kazi za Maendeleo) na kwa kipindi cha Miezi Tisa Programu ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 6,525,331,190** (**TZS Bilioni 1,239,774,760** Mishahara, **TZS Bilioni 1,228,030,730** Matumizi ya Kawaida na **TZS Bilioni 4,057,525,700** kwa Kazi za Maendeleo).

22. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **TZS Bilioni 1,888,859,181** zimepatikana (**TZS Bilioni 1,421,843,314** Mishahara, **TZS Milioni 467,015,867** Matumizi ya Kawaida na hakuna fedha iliyoingia kwa Kazi za Maendeleo) sawa na **asilimia 29** kwa Miezi Tisa na **asilimia 22** kwa Mwaka.

23. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, **Programu Kuu PN0201** kupitia Programu zake ndogo tatu zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

**PROGRAMU NDOGO SN020101: URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI;**

24. **Mheshimiwa Spika;** Progamu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti inasimamiwa na Idara ya Mipango Sera na Utafiti na ina jukumu la kuratibu na kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa Sera, Sheria, Bajeti, Miradi na Mipango ya Taasisi zote zilizomo ndani ya Wizara. Pia, Programu hii inaratibu ufanyaji wa tafiti, ufuatiliaji na kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Vile vile, Programu hii imepewa Jukumu la kuratibu shughuli za Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Ujenzi (DCU).

**25.** **Mheshimiwa Spika;** hadi kufikia Machi, 2025, progaramu ndogo hii imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imeratibu utayarishaji wa Muongozo wa Uthamini na Malipo ya Fidia na Muongozo huo tayari umekamilika kwa ajili ya matumizi.

ii. Imeandaa na kuwasilisha dhana ya Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Uwekaji wa Taarifa za Ardhi kwa Serikali ya KOREA kupitia Kampuni ya Hojung Solution. Aidha, Mradi huo utahusisha ujenzi wa Kituo cha GIS pamoja na kuijengea uwezo Sekta ya Ardhi, Sekta ya Makaazi pamoja na Mipango Miji ambapo kwa sasa Wizara tayari imeshatia saini Hati ya Makubaliano (MoU) ya Mradi huo na Wizara ya Ardhi ya Korea kwa ajili ya utekelezaji.

iii. Imeratibu na kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Wizara ikiwemo Mradi wa Usimamizi na Usajili wa Taarifa za Ardhi (LARIS) pamoja na Ujenzi wa Nyumba za Makaazi ikiwemo Nyumba za Chumbuni na Kiembesamaki, na miradi yote hiyo inaendelea na hatua za utekelezaji.

iv. Imeandaa dhana za Mradi kuhusu kuwajengea uwezo Watendaji wa Wizara katika Sekta ya Ardhi na Makaazi na Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi. Dhana hizo zimeshawasilishwa Shirika la Makaazi Duniani UN-HABITAT ili iweze kusaidia utekelezaji wa dhana hizo pamoja na kudumisha ushirikiano uliopo baina ya Wizara na Shirika hilo.

v. Imeratibu Uandaaji wa Sera ya Miji na Maendeleo ya Makaazi, Rasimu ya Sera hio imekamilika na ipo katika hatua ya kuwasilishwa katika vikao vya maamuzi.

vi. Imeratibu utayarishaji wa Sheria ya usimamizi na Utoaji wa Vibali vya ujenzi, Sheria ya Bodi ya Usajili wa Wathamini, Sheria ya Ofisi ya Mthamini Mkuu na Sheria ya Mabaraza ya Ardhi. Sheria zote hizo zipo katika hatua ya kuwasilishwa katika Vikao vya Maamuzi.

vii. Inaendelea kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Wizara na Taasisi zake ikiwemo Mradi wa Nyumba za Makaazi 72 Mombasa (Kwa Mchina), Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Makaazi na biashara Darajani (Fundi Abduli), Mradi wa matengenezo ya nyumba namba 1699/1705 Mnadani awamu ya kwanza, Mradi wa Jengo la Mkungu Malofa Chakechake Pemba. Miradi hiyo imeshakamilika na baadhi kuuzwa na mengine kukodishwa. Vilevile, imefanya ufuatiliaji wa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi Chumbuni pamoja na Ujenzi wa Ofisi ya Shirika la Nyumba Machomane ambayo bado inaendelea na utekelezaji. Lengo la ufuatiliaji huo ni kuangalia changamoto mbalimbali zinazoikabili miradi hiyo ili iweze kuwekwa Mikakati thabiti ya utatuzi wa changamoto hizo kwa kipindi husika.

viii. Imeratibu na kusimamia suala la uimarishaji wa Mashirikiano na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) kupitia Ziara za

kimafunzo kwa kubadilisha uzoefu wa Kiutendaji baina ya (SJMT na SMZ). Taasisi zilizofaidika na ziara za kimafunzo ni Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali, Mahkama ya Ardhi, Shirika la Nyumba Zanzibar na Kamisheni ya Ardhi. Aidha Wizara hizo zimefanikiwa kusaini hati za makubaliano (MoU) kwa ngazi za Wizara na Ngazi za Kisekta kwa lengo la kua na mpango mzuri wa maeneo ya Mashirikiano.

26. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/25, Programu hii pia imepewa jukumu la kuratibu shughuli za Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Ujenzi (DCU) ambapo Kamati imefanikiwa kufanya shughuli zifuatazo:-

i. Imefanya vikao 18 vya Wataalamu vya kuchambua na kupitisha maombi ya vibali vya ujenzi. Jumla ya vibali 412 vimeombwa na kuchakatwa kati ya hivyo vibali 377 vimekidhi vigezo na kutolewa ambapo Vibali vipya vya ujenzi 262, ujenzi unaoendelea 114 na Kibali kimoja (1) cha matengenezo. Kati ya hivyo vibali 77 ni vya Miradi ya Uwekezaji kupitia ZIPA.

ii. Imefanya ukaguzi wa kawaida kwa maeneo ya ujenzi kwa lengo la kuangalia iwapo wananchi wanajenga kwa kufuata taratibu na Sheria zilizowekwa kulingana na vibali walivyoombea. Aidha, kutokana na ukaguzi huo Kamati imeweza kutoa notisi 620 na kufanya uvunjaji wa misingi maeneo 11 **Kiambanitisho nambari 2 kinafafanua**, kuta zilizojengwa kuziba vichochoro, uvunjaji katika eneo la mtaro Meya,

pamoja na kuvunja vipenu vya maduka yaliyo pembezoni mwa barabara kuu.

27. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/25, Programu hii ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 2,127,000,000** kutokana na Ada za Vibali vya Ujenzi na kwa kipindi cha Miezi Tisa Programu ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1,595,250,000** ambapo hadi kufikia Machi 2025, fedha zilizokusanywa ni **TZS Milioni 368,671,000** sawa na **asilimia 23** ya makadirio ya fedha kwa Miezi Tisa na asilimia **17** ya makadirio ya Mwaka.

28. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, jumla ya **TZS Bilioni 5,836,498,000** ziliidhinishwa kutumika kwa utekelezaji wa Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti (**TZS Milioni 236,498,000** Mishahara, **TZS** Milioni 600,000,000 Matumizi ya Kawaida na **TZS Bilioni 5,000,000,000** kazi za Maendeleo). Na kwa kipindi cha Miezi Tisa Programu hii ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 4,458,053,500** (**TZS Milioni 177,373,500** Mishahara, **TZS Milioni 530,680,000** Matumizi ya Kawaida na **TZS Bilioni 3,750,000,000** Kazi za Maendeleo).

29. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **TZS Milioni 518,858,641** zilipatikana (**TZS Milioni 420,528,641** Mishahara, TZS **Milioni 98,330,000** Matumizi ya Kawaida na hakuna fedha iliyoingia kwa ajili ya Kazi za Maendeleo) sawa na **asilimia 12** kwa Miezi Tisa na **asilimia 9** ya makadirio kwa mwaka.

30. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti itaendelea kuandaa na kuzifanyia mapitio Sera za Wizara ambapo Sera moja itaandaliwa na Sera moja itafanyiwa mapitio (Sera ya Ardhi). Aidha, Sheria 4 zitaandaliwa na kufanyiwa mapitio; Kanuni 5 za utekelezaji wa Sheria za Wizara zitaandaliwa na kufanya tafiti 2. Pia, itaendelea kukusanya takwimu za Sekta ya Ardhi, Makaazi na Nyumba; itafanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Miradi na Programu za Wizara; itasimamia shughuli za DCU na kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi.

31. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 2,610,010,427** kutokana na mapato yatokanayo na utoaji wa Vibali vya ujenzi.

32. **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Programu kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 36,629,195,000** ambapo **TZS Milioni 260,795,200** Mishahara, **TZS Milioni 803,400,000** Matumizi ya kawaida na **TZS Bilioni 35,565,000,000** kwa kazi za Maendeleo.

**PROGRAMU NDOGO SN020102: UTAWALA NA UENDESHAJI.**

33. **Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ina jukumu la kusimamia uendeshaji wa

shughuli za Wizara, usimamizi wa rasilimali watu kwa kuandaa Mipango ya kuwajengea uwezo Watumishi, kuimarisha mazingira bora ya kazi, kushughulikia haki na stahiki za Watumishi, kuhakikisha upatikanaji wa Watendaji wa kutosha na wenye sifa ndani ya Wizara na Taasisi pamoja na kusimamia nidhamu kwa watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Hadi kufikia Machi, 2025, imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imelipa stahiki za Wafanyakazi 28 (wafanyakazi 14 wamelipwa posho la likizo, Wafanyakazi kumi (10) wamelipwa posho la kufanya kazi maalum, Mfanyakazi mmoja (1) amelipwa stahiki yake ya posho la ufiwa na Wafanyakazi watatu (3) wamepatiwa posho la kufanya kazi baada ya saa za kazi (overtime). **Kiambatanisho nambari 3 Kinafafanua.**

ii. Imegharamia mafunzo ya muda mrefu Mfanyakazi 1 na Wafanyakazi 34 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuwaongezea ujuzi wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. **Kiambatanisho nambari 4 (a) na 4 (b) kinafafanua.**

iii. Imetengeneza Habari 31 na kuzirusha hewani kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Aidha, Makala 5 zimeandaliwa kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya utekelezaji wa shughuli za Wizara.

iv. Imesimamia upatikanaji wa huduma za kiofisi ikiwemo malipo ya umeme, vifaa vya kuandikia, ulinzi, usafi na

upatikanaji wa maji safi na salama, kwa lengo la kuhakikisha shughuli za Wizara zinatekelezwa kwa ufanisi.

v. Imesimamia upatikanaji wa usafiri kwa kazi za Ofisi kwa ajili ya shughuli za Ofisi kwa kufanya matengenezo ya vyombo vya usafiri na ununuzi wa mafuta.

vi. Imesimamia uajiri wa Watumishi watatu (03) ambao ni Mwanasheria, Mthamini Msaidizi na Afisa TEHEMA. Vilevile, imefanya upimaji wa Watumishi 90 ambapo wote walipatiwa nyongeza za Mshahara pamoja na Mtumishi mmoja kupandishwa Daraja baada ya kurudi masomoni.

vii. Imesuluhisha na kuipatia ufumbuzi migogoro ya ardhi 16 kati ya 44 iliyowasilishwa kupitia Kamati ya Usuluhishi wa Migogoro na kufuatilia maeneo yenye migogoro hiyo. Aidha jumla ya hoja na changamoto 76 zimepatiwa ufumbuzi kati ya hoja 78 zilizowasilishwa na wananchi kupitia Mfumo wa Sema na Rais Mwinyi (SNR).

viii. Imeendelea kusimamia Miundombinu ya TEHAMA ya Wizara pamoja na uboreshaji wa Kitengo cha TEHAMA kwa kuandaa ripoti moja ya Tathimini juu ya uboreshaji Miundombinu ya TEHAMA ya Wizara na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA.

34. **Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha 2024-2025 Programu hii iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 1,821,936,000** (TZS Bilioni 1,416,535,000 Mshahara

na TZS Milioni 405,000,000 Matumizi ya Kawaida). Kwa kipindi cha Miezi Tisa Programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 1,383,871,460** (TZS Bilioni 1,062,401,460 Mishahara na TZS Milioni 321,470,000 Matumizi ya Kawaida).

**35.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi 2025, fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 873,525,561** (TZS Milioni 680,872,361 Mishahara na TZS Milioni 192,653,200 Matumizi ya Kawaida) sawa na asilimia **63** ya makadirio kwa Miezi Tisa na asilimia **48** kwa mwaka.

**36.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu ndogo ya Uendeshaji na Utumishi itaratibu shughuli za uendeshaji na usimamizi wa rasilimali za Wizara; itasimamia uajiri Wafanyakazi 04; itafanya upimaji wa Watendaji kwa Wafanyakazi 90; itawajengea uwezo wafanyakazi (58) kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu (05) na muda mfupi (55) na kuwapatia stahiki zao kwa mujibu wa taratibu za Utumishi; itafanya mapitio ya Mkataba wa huduma kwa wateja na itaratibu mapitio ya miundo na majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa kazi na kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara.

**37.** **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 2,053,245,200** kati ya hizo **TZS Bilioni**

**1,440,835,000** Mishahara na **TZS Milioni 612,410,200** Kazi za Kawaida.

**PROGRAMU NDOGO SN020103: URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA.**

**38. Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia Utawala na Mipango ya kazi zote za Wizara kwa upande wa Pemba ikiwemo Programu na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2025, Programu hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imetoa jumla ya fomu 96 za maombi ya hati za usajili wa Kondominio ambapo fomu 47 zilijazwa na kurejeshwa, kati ya hizo fomu 23 zilikidhi vigezo na kusajiliwa. Aidha, Hati 8 zilitolewa baada ya kukamilika malipo ya hati zilizosajiliwa.

ii. Imesajili Ramani saba za Miradi ya Kondominio katika Wilaya 3 za Pemba (Chake Chake, Micheweni na Mkoani).

iii. Imesajili Majengo 5 ya Kondominio kwa Wilaya 3 za Pemba (Chake Chake, Micheweni na Mkoani).

iv. Imefanya ufuatiliaji wa kazi za Ofisi na Miradi ya Maendeleo na kufanya Ziara ikiwemo Afisi ya Manispaa Chake Chake, eneo la Utambuzi Makangale, Eneo la Shirika la Nyumba linalotarajiwa kujengwa nyumba za kisasa lililopo Finya, Eneo la

Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi Makaani Kojani, Mradi wa ujenzi wa Jengo la Biashara na Makaazi uliopo Mabatini ChakeChake kwa lengo la kuangalia mafanikio na changamoto na kuweka Mikakati ya utatuzi wa changamoto hizo.

v. Imepokea migogoro mipya 5 ambapo Afisi kuu iliendelea kusikiliza migogoro hiyo pamoja na ya awali na kuweza kuitolea maoni migogoro 8 na migogoro 9 inaendelea na ufuatiliaji.

vi. Imewapatia stahiki zao Wafanyakazi Sabini na Sita (76) ikiwemo malipo ya safari kwa Wafanyakazi 61, Wafanyakazi watatu (3) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu (2) ngazi ya Degree na Mfanyakazi 1 Shahada ya Pili (Master), Mfanyakazi mmoja (1) amepatiwa mafao ya ufiwa, imelipa likizo kwa Wafanyakazi (5) na Wafanyakazi watano (5) wamepatiwa posho la malipo baada ya saa za kazi.

vii. Imefanya matengenezo ya Vyombo vya usafiri, ununuzi wa vifaa na huduma za uendeshaji wa Ofisi vikiwemo umeme, mafuta pamoja na vifaa vya kuandikia.

viii. Imefanya vikao vitano (5) vikiwemo vya uwajibikaji kazini na vikao vya kutathimini utekelezaji wa Mpango kazi wa Wizara.

39. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/25, Afisi kuu Pemba kupitia Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Ujenzi (DCU) imefanikiwa kufanya shughuli zifuatazo:-

i. Imepokea maombi ya vibali vya ujenzi 15 (Serikali 3 na Wananchi 12) katika maeneo mbalimbali ya Pemba.

ii. Imefanya ukaguzi wa udhibiti wa ujenzi katika maeneo mbalimbali ikiwemo maeneo ya Uwekezaji Makangale- Wilaya ya Micheweni, Chake Chake maeneo 6, Mkoani eneo 1, Micheweni eneo 1, eneo linaloombwa kwa ajili ya ujenzi wa Mabanda ya Kambi ya Mkandarasi (Propav Company Limited) wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba na eneo linalojengwa Kiwanja cha Michezo cha Gombani kwa lengo la kuangalia masharti ya uombaji wa vibali kamam yamezingatiwa.

40. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu hii ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 43,000,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa mwaka na ilipangiwa kukusanya **TZS Milioni 33,599,997** kwa kipindi cha Miezi Tisa.

41. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **TZS Milioni 18,034,800** zimekusanywa sawa na **asilimia 54** ya makadirio ya Miezi Tisa na **asilimia 42** ya mwaka.

42. **Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Milioni 864,936,000 (TZS Milioni 419,836,000** Mishahara na **TZS Milioni 445,100,000** Matumizi ya Kawaida). Kwa kipindi cha Miezi Tisa, Programu hii

ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Milioni 626,266,067** (**TZS Milioni 271,973,907** Mishahara na **TZS Milioni 354,292,160** Matumizi ya Kawaida).

**43. Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, fedha zilizotumika ni jumla ya **TZS Milioni 560,928,960** (**TZS Milioni 420,685,626** Mishahara sawa na **asilimia 154** ya fedha zilizopangwa kwa Miezi Tisa na **asilimia 100** kwa Mwaka na **TZS Milioni 140,243,334** Matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 39** ya fedha zilizopangwa kwa Miezi Tisa na **asilimia 32** kwa Mwaka.

**44. Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu ya Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba itaendelea kuratibu shughuli za Wizara Pemba; itaimarisha upatikanaji wa Makaazi bora na nafuu kwa wananchi, itasimamia shughuli za DCU, itaimarisha kazi na usimamizi wa Mipango, Bajeti, na Ufuatiliaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa upande wa Pemba, itaimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi, itawapatia mafunzo ya muda mfupi Wafanyakazi 05, mafunzo ya muda mrefu Wafanyakazi 04 na itasimamia ajira mpya kwa Wafanyakazi 15.

**45. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu hii imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 115,800,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

**46. Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS**

**Bilioni 1,283,464,200** ambapo **TZS Milioni 444,138,200** Mishahara na **TZS Milioni 839,324,000** Kazi za Kawaida.

47. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, **Programu Kuu PN0201** ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 2,725,810,427** kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

48. **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Programu Kuu PN0201 ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 39,965,904,600** ambapo **TZS Bilioni 2,145,768,600** Mishahara, **TZS Bilioni 2,255,136,000** Kazi za Kawaida na **TZS Bilioni 35,565,000,000** Kazi za Maendeleo.

## PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI

49. **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu PN0202 ya Usimamizi wa Ardhi ina jukumu la kuhakikisha usalama na umiliki wa matumizi ya ardhi Nchini (Security of Land Tenure), Programu hii ina Programu ndogo moja, ambapo kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, ilikadiriwa kukusanya **TZS Milioni 510,000,000** na **TZS Milioni 382,500,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa.

50. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **TZS Milioni 159,958,459** zilikusanywa sawa na asilimia **42** kwa Miezi Tisa na asilimia **31** kwa mwaka.

51. **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu Kuu PN0202 ya Usimamizi wa Ardhi iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 4,003,499,000** (**TZS Milioni 363,699,000** Mishahara, **TZS Bilioni 3,003,300,000** Ruzuku ya Mishahara **TZS Milioni 256,400,000** Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida na TZS Milioni 380,100,000 kwa Matumizi ya Kawaida OC) na **TZS Bilioni 2,891,089,250** ni makisio ya fedha kwa kipindi cha Miezi Tisa (**TZS Milioni 272,774,250** Mishahara, **TZS Bilioni 2,289,150,000** Ruzuku ya Mishahara **TZS Milioni 193,840,000** ni Ruzuku na **TZS Milioni 135,325,000** kwa Matumizi ya Kawaida).

52. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025 fedha zilizopatikana ni **TZS Bilioni 2,708,908,507** (**TZS Milioni 303,603,275** Mishahara, **TZS Milioni 70,550,000** Matumizi ya Kawaida, **TZS Bilioni 2,270,555,233** Ruzuku ya Mishahara na **TZS Milioni 64,200,000** ni Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida) sawa na **asilimia 94** kwa Miezi Tisa na **asilimia 68** kwa mwaka.

## PROGRAMU NDOGO SN020201: USIMAMIZI WA ARDHI

53. **Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi inatekelezwa na Taasisi Tatu (3) za Wizara ambazo ni Mahkama ya Ardhi, Kamisheni ya Ardhi na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi ilitekeleza shughuli zote zinazohusiana na masuala ya Ardhi kupitia Taasisi zake kama ifuatavyo:-

## HN02020108: UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

**54.** **Mheshimiwa Spika;** Huduma hii inatekelezwa kupitia Mahkama ya Ardhi ambayo imeanzishwa chini ya Sheria Namba 7 ya Mwaka 1994 kwa lengo la kupokea, kusikiliza na kuyatolea uamuzi mashauri yanayotokana na migogoro ya ardhi yanayowasilishwa na Wananchi.

**55.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, Huduma imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imepokea kesi mpya Mia Moja na Sabini (170) ambazo zimefunguliwa katika Mahkama za Unguja na Pemba. Aidha, Mahkama imeendelea kusikiliza kesi hizo pamoja na za awali ambapo kesi Mia Moja na Arubaini (140) zimetolewa uamuzi. **Kiambatanisho nambari 5 Kinafafanua.**

ii. Imeendelea kutoa elimu kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa jamii katika Mkoa wa Kusini Unguja ikiwemo Kizimkazi Mkunguni, Kizimkazi dimbani na Mtende, Mkoa wa Kaskazini Unguja eneo la Gamba na Mkoa wa Mjini Magharibi katika eneo la Chukwani kupitia ushiriki wa 'Legal Aids Campaign' kwa mashirikiano makubwa na Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora pamoja na Mahkama Kuu.

Mafunzo hayo yalihusu ufafanuzi wa Kisheria juu ya mwenendo wa kesi za ardhi Mahkamani, kuifahamu Mahkama ya Ardhi na kazi zake, kutatua migogoro ya ardhi kwa njia ya usuluhishi na faida zake, namna

ya kumiliki ardhi kwa mujibu wa Sheria pamoja na kushajiisha wananchi kusajili ardhi zao ili kuepuka migogoro ya ardhi. Pia, elimu hiyo imetolewa kupitia Maonesho ya Siku ya Sheria Zanzibar pamoja na kipindi maalumu cha "Televisheni" kilichorushwa moja kwa moja (live) na ZCTV.

iii. Imelipa Stahiki kwa Wafanyakazi 14 ambapo Wafanyakazi 9 wamelipwa posho la malipo ya saa za ziada, Wafanyakazi watatu (03) wamelipwa Ubani wa kufiwa, Mfanyakazi mmoja (01) amepatiwa mafunzo ya muda mrefu na Mfanyakazi mmoja (01) amepatiwa posho ya likizo. Vilevile, imefanya matengenezo ya Vyombo vya usafiri, ununuzi wa vifaa na huduma za uendeshaji wa Ofisi vikiwemo umeme, mafuta pamoja na vifaa vya kuandikia.

56. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mahkama ya Ardhi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 10,000,000** na kwa kipindi cha Miezi Tisa Mahkama ilikadiria jumla ya **TZS Milioni 7,500,000** kupitia chanzo chake cha Ada ya (Migogoro ya Ardhi na Migogoro ya Kodi za Nyumba).

57. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **TZS Milioni 7,393,700** zilikusanywa ambayo sawa na asilimia **99** ya makadirio kwa Miezi Tisa na asilimia **73** kwa mwaka.

58. **Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Matumizi Mahkama ya Ardhi ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Milioni**

**743,799,000** (**TZS Milioni 363,699,000** Mishahara na **TZS 380,100,000** kwa Matumizi ya Kawaida) na Kwa upande wa Miezi Tisa jumla ya **TZS Milioni 444,774,250** ziliidhinishwa (**TZS Milioni 129,344,250** Mishahara na **TZS Milioni 315,430,000** Matumizi ya Kawaida).

59. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 374,153,275** (**TZS Milioni 303,603,275** Mishahara na **TZS Milioni 70,550,000** Matumizi ya Kawaida) sawa na **asilimia 84** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 50** kwa mwaka.

60. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Mahkama ya Ardhi kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi itaendelea kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri yanayohusiana na migogoro ya ardhi iliyowasilishwa Mahakamani; itayatolea uamuzi mashauri 300 (Unguja 200 na Pemba 100); itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu migogoro ya ardhi na itaendelea kujenga mazingira bora ya kazi.

61. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Mahkama ya Ardhi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 15,000,000** kutokana na Ada ya Mahkama.

62. **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Mahkama ya Ardhi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 787,999,200** ambapo **TZS Milioni 387,999,200** Mishahara na **TZS Milioni 400,000,000** Matumizi ya Kawaida.

## HN02020107: KUSIMAMIA NA KUIDHINISHA RIPOTI ZA UTHAMINI

63. **Mheshimiwa Spika;** Huduma hii ipo chini ya Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi na inatekelezwa na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ambayo imeanzishwa kwa Sheria Namba 5 ya Mwaka 2015 kwa madhumuni ya kuhakikisha usimamizi mzuri wa uthaminishaji wa mali kwa malengo mbalimbali ya Sekta ya Umma, Biashara na Wananchi kwa ujumla. Kazi kuu ya Mthamini Mkuu wa Serikali ni kuthibitisha kazi za uthamini zinazofanywa Nchini na Wathamini wa Taasisi za Serikali na Taasisi binafsi.

64. **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Huduma imetekeleza kazi zifuatazo:-

    i. Imethibitisha ripoti 331 kati ya hizo 15 ni ripoti za uthamini mali kwa ajili mikopo (Morgage Purpose), 56 ripoti za uthamini mali kwa ajili ya thamani (Market Value Determination), 193 ripoti za uthamini mali kwa ajili ya mirathi (Inheritance Purpose), 67 ripoti za uthamini mali kwa ajili ya fidia (Compensation Purpose).

    ii. Imeandaa Miongozo ya uthamini kwa mujibu wa Sheria, ambapo imetayarisha Muongozo wa Uthamini wa Mali na Malipo ya Fidia Zanzibar ambao utasaidia kupunguza changamoto za uthamini hasa uthamini wa fidia. Muongozo huu umekamilika na upo tayari kwa matumizi. Muongozo huu pia ndani yake umejumisha

miongozo mitatu ambayo ni Muongozo wa masafa ya Miti na Mazao, Muongozo wa Viwango vya Gharama za Ujenzi na Muongozo wa Haki ya Matumizi ya Ardhi.

iii. Imefanya uthamini wa Mali (Fixed and non fixed Assets) katika Taasisi za Serikali ili kufahamu thamani za Mali za Taasisi hizo (Book Value Determination) kwa ajili kuweka thamani halisi za Serikali kwenye Asset Register za Msajili wa Hazina ambapo ni muhimu kujua aina, idadi, uchakavu na thamani za soko za mali kwa kipindi maalum zinazomilikiwa na Taasisi mbalimbnali za umma Nchini.

iv. Inaendelea na marekebisho ya Sheria ya Ofisi ya Mthamini Mkuu na Bodi ya Usajili wa Wathamini Zanzibar ili kuweka usimimizi mzuri zaidi wa kazi za uthamini Nchini. Sheria hizo zipo katika hatua za kuwasilishwa katika vikao vya maamuzi.

v. Imetoa elimu ya Uthamini kwa wadau kupitia Mikutano na Vyombo vya habari kuhusu masuala ya Uthamini ikiwemo umuhimu wa uthaminishaji Mali kwa malengo tofauti hasa katika uthamini wa Fidia, Uthamini kwa ajili ya pango, Uthamini kwa ajili ya Mikopo Benki na Uthamini kwa ajili ya Mirathi.

**65.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu hii kupitia Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 500,000,000**

na **TZS Milioni 375,000,000** ilikadiriwa kukusanya kwa kipindi cha Miezi Tisa kutokana na chanzo chake cha mapato ya Ada ya Uthamini.

66. **Mheshimiwa Spika**; Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **TZS Milioni 152,564,759** zilikusanywa sawa na **asilimia 41** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 31** ya makadirio kwa mwaka.

67. **Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Matumizi Ofisi ilipangiwa kutumia Ruzuku ya jumla ya **TZS Milioni 256,400,000** kwa mwaka na **TZS Milioni 193,840,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa.

68. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 64,200,000** sawa na **asilimia 33** ya makadirio ya Fedha zilizopangwa kwa Miezi Tisa na **asilimia 25** kwa mwaka.

69. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi itahakiki na kuidhinisha ripoti 610 za uthamini wa rasilimali; itaendelea kusajili na kuwapatia leseni Wathamini 60, Kusambaza na kutoa elimu juu ya Muongozo wa Uthamini wa Mali na Malipo ya Fidia, itatoa elimu ya Uthamini kwa Wadau mbalimbali wenye uhitaji wa uthamini wa fidia kupitia Vyombo vya habari pamoja na Mikutano kwa Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi, Ofisi itaendelea kuweka kumbukumbu za

ripoti za uthamini wa mali zilizofanyiwa Uthamini katika Mfumo na itakamilisha marekebisho ya Sheria ya Ofisi ya Mthamini Mkuu na Bodi ya Usajili wa Wathamini Zanzibar kwa kuzipeleka katika vyombo vya maamuzi.

**70.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi chini ya huduma ya Kusimamia na Kuidhinisha Ripoti za Uthamini imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 520,000,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

**71.** **Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi chini ya huduma ya Kusimamia na Kuidhinisha Ripoti za Uthamini iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako kuidhinisha Ruzuku ya jumla ya **TZS Milioni 507,700,000** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida.

**HN02020101: UPANGAJI NA USIMAMIZI WA ARDHI**

**72.** **Mheshimiwa Spika;** Huduma hii ya Progaramu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi inatekelezwa na Kamisheni ya Ardhi ambayo imeanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2015 kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria za Sekta ya Ardhi na kuziunganisha Idara zote zinazosimamia matumizi na maendeleo ya ardhi. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Huduma imetekeleza kazi zifuatazo:-

1. Imetayarisha jumla ya Hati za Haki ya Matumizi ya Ardhi 1,146 (879 Unguja na 267 Pemba) na kupewa

Wananchi. Aidha, jumla ya Mikataba ya ukodishaji wa Ardhi 261 Unguja imetayarishwa kwa ajili ya kuwapatia umiliki wa Ardhi kwa Wawekezaji kwa njia ya ukodishwaji na Mikataba ya Ardhi 128 (Unguja 85 na Pemba 43) imehakikiwa na maeneo 71 ya uwekezaji Unguja yamefanyiwa ukaguzi kwa lengo la kubaini eneo lilipo na aina ya uwekezaji unaotaka kufanyika.

2. Imeandaa jumla ya hati za Eka tatu 466 kutokana na maombi ya Wananchi ya uhitaji wa kurithishwa eka hizo kutoka kwa Wazee wao na kukagua Mashamba 73 ya Eka tatu Unguja kwa lengo la kubaini hali halisi ya Eka hizo.

3. Imefanya kazi za Uthamini kwa maeneo 1,107 (715 Unguja na 392 Pemba) kwa ajili ya Mirathi, Fidia na kutambua thamani ya Soko la sasa pamoja na kufanya Utambuzi kwa Viwanja 3,407 (2,429 Unguja na 978 Pemba).

4. Jumla ya maombi 919 (669 Unguja na 250 Pemba) yamewasilishwa na kujadiliwa kwa ajili ya uhaulishaji, ambapo maombi 746 (582 Unguja na 164 Pemba) yamekubaliwa na kufanyiwa uhaulishaji. Aidha, maombi 74 (55 Unguja 19 Pemba) yamekataliwa kwa kutokidhi vigezo na 99 (32 Unguja na 67 Pemba) yamerejeshwa kwa Wahusika kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho ya kukamilisha vielelezo.

5. Imepima maeneo 1,556 (1,126 Unguja na 430 Pemba) kati ya hayo maeneo 40 ni kutokana na maombi ya Taasisi za Serikali na maeneo 1,086 kutokana na maombi

ya Wananchi pamoja na kupima vianzio vya upimaji 47 (14 Unguja na 33 Pemba).

6. Taarifa tisa (09) za Vipimo vya kupwa na kujaa kwa Maji ya Bahari (Tide Gauge) zimerikodiwa kwa ajili ya matumizi ya usafiri baharini kwa kupata viashiria vya hali ya hatari, matumizi ya upatikanaji wa taarifa za Tafiti na kujua hali halisi la ongezo la mawimbi ya bahari yanayoaathiri mmong'onyoko wa Ardhi.

7. Imefanikiwa kutoa nambari 1,376 (882 Unguja na 494 Pemba) za ZUPIN (Zanzibar Identification Percel Number) ambazo ni nambari maalumu zinazotumika katika utengenezaji wa Hati na kuondosha changamoto ya kuwa na uwiano wa nambari katika Hati pamoja kuandaa ripoti 1,173 (846 Unguja na 327 Pemba) ya hali ya upimaji zinazotoka katika vifaa maalumu GPS.

8. Imeandaa na kutoa Miongozo ya Matumizi ya Ardhi 2,184 (1,809 Unguja na 375 Pemba) Miongozo hiyo hutumika katika utaratibu wa upatikanaji wa vibali vya ujenzi, upimaji na uhaulishaji.

9. Inaendelea na zoezi la ukusanyaji wa taarifa za Kijiografia katika uimarishaji na upangaji wa Vijiji vilivyokaribu na Maeneo ya uwekezaji (EPZ) katika kijiji cha Dimani Unguja.

.

10. Imehakiki na kusajili maeneo 876 (667 Unguja na 209 Pemba) kwa ajili ya kuweka kumbukumbu haki za umiliki.

11. Imeimarisha mazingira ya kazi kwa kuipatia Ofisi vitendea kazi vikiwemo Vifaa vya kuandikia, Huduma ya Usafi, Huduma ya Umeme, Ununuzi wa vifaa vya ICT, ununuzi wa Samani za Ofisi, Wino pamoja na kufanya matengenezo ya gari na matengenezo madogo madogo katika jengo la Kamisheni Unguja na kufanya matengenezo makubwa katika Jengo la Afisi ya Kamisheni Pemba.

12. Imewapatia Stahiki zao za likizo Wafanyakazi Unguja na Pemba, mafunzo ya muda mfupi Wafanyakazi 42 (27 Unguja na 15 Pemba) na Wafanyakazi 242 (Unguja 175 na Pemba 67) wamepatiwa mafunzo ya ndani. Wafanyakazi 196 (Unguja 146 na Pemba 50) wamepatiwa mafunzo ya masuala Mtambuka, Kanuni za Utumishi. Wafanyakazi Kumi na Tatu (13) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani ya Upangaji wa Ardhi baharini (Hydrodraphic Suvey) na Utunzaji wa Kumbumbu.

13. Imefanya vikao Vinane (08) vya Bodi ya Utendaji na Usimamizi wa Kamisheni ya Ardhi.

14. Imeandaa jumla ya vipindi 35 vya uelimishaji jamii juu ya Sheria za Ardhi na kurushwa hewani kupitia ZBC Redio na ZBC TV.

15. Imefanya Mikutano 11 ya Kliniki ya Ardhi katika Shehia za Pwani Mchangani, Ukongoroni, Makunduchi Nganani, Maungani, Bumbwini na Mtende Unguja na Machomane, Wara, Wawi, Micheweni, Kangagani na Mjini Ole Pemba kwa lengo la kutoa elimu, kusikiliza

changamoto za Wananchi zinazohusiana na masuala ya ardhi pamoja na kutatua migogoro ya ardhi.

73. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi kupitia huduma ya Upangaji na Usimamizi wa Ardhi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 6,224,320,746** na kwa kipindi cha Miezi Tisa ilikadiriwa kukusanya **TZS Bilioni 4,668,202,512** kutokana na Ada ya Uthamini, Muongozo wa Matumizi ya Ardhi, Nyaraka za Ardhi, Upimaji wa Ardhi, Usajili wa Ardhi na Uhaulishaji wa Ardhi.

74. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, Programu ilifanikiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 5,435,353,178** sawa na **asilimia 116** kwa Miezi Tisa na **asilimia 87** ya Mwaka.

75. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi kupitia huduma ya Upangaji na Usimamizi wa Ardhi ilikadiriwa kutumia **TZS Bilioni 4,645,092,394/=.** Kati ya hizo Matumizi ya kawaida yatokanayo na makusanyo (50%) ni **TZS Bilioni 2,355,942,394/=** na Ruzuku ya Mshahara **TZS Bilioni 2,289,150,000.**

76. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, fedha zilizopatikana ni **TZS Bilioni 4,988,231,821** sawa na **asilimia 107%** ya makadirio, (Kati ya hizo **TZS Bilioni 2,717,676,589** ni Matumizi ya Kawaida ambayo yanatokana na makusanyo ya 50% na T**ZS Bilioni 2,270,555,232** ni Ruzuku ya Mishahara).

**77. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi chini ya Huduma ya Upangaji na Usimamizi wa Ardhi imepanga kuimarisha upatikanaji wa Hati za Haki ya Matumizi ya Ardhi 2,500 (Unguja 1,500 na Pemba 1,000), kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa Ardhi 480 (Unguja 400 na Pemba 80), kuratibu na kufanya Uthamini wa maeneo ya Ardhi 2,400 (Unguja 2000 na Pemba 400), kufanya Utambuzi wa Ardhi kwa meneo 10 (Unguja 06 na 04 Pemba) na kutambua viwanja 8,500 (Unguja 6,000 na Pemba 2,500), kufanya ukaguzi na uhaulishaji wa maeneo 2,700 (Unguja 2,400 na 300 Pemba), Kuendeleza na zoezi ya kampeni ya kamilisha Uhaulishaji, kuendelea na upimaji wa mipaka ya maeneo ya Serikali 400 Unguja 300 na 100 Pemba na maeneo yanayotakana na maombi ya Wananchi 2,250 (Unguja 1,300 na Unguja 950) kukamilisha utekelezaji wa agizo la kupanga na kupima mji wa Kojani.

**78. Mheshimiwa Spika;** Aidha, programu kupitia Kamisheni ya Ardhi imepanga kuendela uayarishaji wa ramani za msingi za ardhini (base map) 14 (Unguja 10 na Pemba 04) na taarifa za (Tide Gauge) pamoja na kuandaa na kusimamia alama msingi za Upimaji, kutayarisha nambari za ZUPIN na ramani kwa ajili ya hati na uwekaji wa kumbukumbu za upimaji na ramani, kupanga na kusimamia Maendeleo ya Miji Zanzibar kwa kupanga Miji 6 (Unguja 04 na Pemba 02) na Maendeleo ya miji midogo ya Zanzibar kwa kupanga miji midogo 06 (Unguja 4 na 2 Pemba ), kuhakikisha uwepo wa mpango wa usimamizi na upangaji wa maeneo ya baharini (Marine

Spatial Plan), kubainisha, kuhakiki na kuyatangaza maeneo ya Ardhi ya akiba (land bank) na kutayarisha mpango wa kina kwa ajili ya Ardhi ya akiba na kuimarisha mipango ya Maendeleo kwa Vijiji ambavyo vipo karibu na EPZ.

79. **Mheshimiwa Spika;** vilevile, Progaramu itaendelea na Kusajili maeneo 1,600 (Unguja 1,100 na Pemba 500) yaliyokamilisha vigezo vya kusajiliwa na kuhakiki maeneo yaliyosajiliwa, kuimarisha mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu za usajili , kufanya uhamasishaji kwa jamii kupitia Kliniki ya Ardhi, Kuimarisha mazingira bora ikiwemo vifaa na samani za Ofisi na uimarishaji wa huduma, upatikanaji wa stahiki za wafanyakazi na kuwajengea uwezo wa kitaaluma, kuendelea na kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni, uandaaji wa mipango ya muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi pamoja na kufanya Tafiti zinazohusu masuala ya Ardhi na kubuni miradi kuhusu masuala ya Ardhi na kuendelea na utayarishaji wa Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Ardhi.

80. **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi kupitia Huduma ya Upangaji na Usimamizi wa Ardhi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 10,164,108,136** kutoka vyanzo vya mapato.

81. **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Programu Kuu **PN0202** ya Usimamizi wa Ardhi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza

lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 4,360,699,200** ambapo **TZS Bilioni 3,065,000,000** Ruzuku ya Mshahara, **TZS Milioni 387,999,200** Mshahara, **TZS Milioni 400,000,000** Matumizi ya Kazi za Kawaida na **TZS Milioni 507,700,000** Ruzuku ya Matumizi ya Kazi za Kawaida.

**82.** **Mheshimiwa Spika;** Vile vile, naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya **asilimia 50** ya makusanyo ya mapato ya Kamisheni ya Ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za kawaida.

## PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI

**83.** **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu PN0203 ya Maendeleo ya Makaazi ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa makaazi bora, salama, jumuishi na endelevu kwa wananchi pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa Wawekezaji wa Sekta Umma na Binafsi katika huduma ya Makaazi.

**84.** **Mheshimiwa Spika;** Programu hii kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, ilikadiriwa kukusanya **TZS Bilioni 1,590,000,000** na **TZS Bilioni 1,192,500,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa.

**85.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, **TZS Bilioni 1,087,005,712** zilikusanywa sawa na **asilimia 91** kwa Miezi Tisa na **asilimia 68** kwa Mwaka.

**86.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu Kuu **PN0203** ya Maendeleo ya Makaazi iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 40,536,432,000**

(**TZS Milioni 176,532,000** Mishahara, **TZS Milioni 254,900,000** Matumizi ya Kazi za Kawaida, **TZS Milioni 105,000,000** Ruzuku ya Matumizi ya Kazi za Kawaida na **TZS Bilioni 40,000,000,000** kazi za Maendeleo) na **TZS Bilioni 30,424,789,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa.

87. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi 2025, fedha zilizopatikana ni **TZS Bilioni 24,349,107,380** (**TZS Milioni 128,818,710** Mishahara, **TZS Milioni 86,780,800** Matumizi ya Kazi za Kawaida, **TZS Milioni 48,390,000** Ruzuku ya Matumizi ya Kazi za Kawaida na **TZS Bilioni 24,085,117,870** kazi za Maendeleo) sawa na **asilimia 80** kwa Miezi Tisa na **asilimia 60** kwa mwaka.

88. **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu PN0203 inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Makaazi, Shirika la Nyumba Zanzibar na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya ya Kondominio na Huduma ya Utatuzi wa Migogoro kwa Wapangaji wa Nyumba. Programu hii ina Programu ndogo moja SN020301 ya Maendeleo ya Makaazi.

**PROGRAMU NDOGO SN020301: MAENDELEO YA MAKAAZI**

**HUDUMA HN02030102: USAJILI WA MAJENGO NA JUMUIYA YA KONDOMINIO.**

89. **Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo ya SN020301 kupitia huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya ya

Kondominio inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Makaazi ambayo ina jukumu la kusimamia Maendeleo ya Makaazi, kusajili Majengo ya Kondominio, kuratibu upatikanaji wa Makaazi bora na nafuu kwa Wananchi pamoja na kusimamia matumizi ya pamoja kwa majengo yenye sehemu zinazomilikiwa na mtu zaidi ya mmoja. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu ndogo kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya ya Kondominio imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imetoa jumla ya fomu Mia Moja Sabini na Mbili (172) za maombi ya usajili wa Kondominio ambapo fomu 165 zilijazwa, zilikidhi vigezo, zilisajiliwa na kutolewa Hati.

ii. Imesajili Ramani Kumi na Mbili (12) za miradi ya Kondominio **Kimabatanisho nambari 6 kinafafanua.**

iii. Imesajili Majengo/Miradi ya Kondominio (Condominium Registration) kwa Miradi Kumi na Mbili (12).

iv. Imesajili Umiliki wa Sehemu/fleti (Unit Registration) Mia Moja Themanini (180) za Nyumba za Kondominio katika maeneo ya Michenzani, Kilimani, Mapinduzi, Machomane, Mbuyuni, Madungu, Paje, Jambiani, Mbweni, Malindi, Uroa, Kiwengwa, Kikwajuni, M/kwerekwe na Kwahani.

v. Imefanya ukaguzi wa miradi ya Kondominio Ishirini na nne (24) kwa lengo hatua iliyofikiwa baada

ya kusajili na utekelezaji wa masharti na vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa usajili . **Kiambatisho nambari 5 kinafafanua.**

vi. Imeendelea kusimamia ujenzi wa mradi wa nyumba za Makaazi Chumbuni.

vii. Imeendelea na zoezi la utoaji wa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu usajili wa fleti za Kondomonio na uanzishwaji wa Jumuiya za Kondominio kwa wamiliki na wakaazi wa Nyumba za Maendeleo Mtemani na Wete-Pemba pamoja na Shehia Nane (8) kwa Unguja ambazo ni Kisima Majangoo, Kisiwandui, Mwembe Tanga, Kwahani Mlandege, Rahaleo, Mwembeshauri na Miembeni ambapo wananchi wamehamasika na wanaendelea kujisajili.

viii. Imenunua vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ikiwemo vifaa vya Tehema, Samani na Vifaa vya kuandikia.

**90.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1,590,000,000** na **TZS Bilioni 1,192,500,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa.

**91.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, Programu imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1,087,005,712** sawa na **asilimia 91** kwa Miezi Tisa na **asilimia 68** ya makadirio kwa mwaka.

92. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya ya Kondominio ilipangiwa kutumia **TZS Bilioni 40,431,432,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Kazi za Kawaida, Mishahara na Maendeleo (**TZS Milioni 176,532,000** Mishahara, **TZS Milioni 254,900,000** Matumizi ya Kawaida, na **TZS Bilioni 40,000,000,000** Kazi za Maendeleo) na **TZS Bilioni 30,346,039,000** ilipangiwa kutumia kwa kipindi cha Miezi Tisa (**TZS Milioni 152,399,000** Mishahara, **TZS Milioni 213,640,000** Matumizi ya kawaida na **TZS Bilioni 30,000,000,000** Kazi za Maendeleo).

93. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, fedha zilizopatikana ni **TZS Bilioni 24,300,717,380** (**TZS Milioni 128,818,710** Mishahara, **TZS Milioni 86,780,800** Matumizi ya Kazi za Kawaida na **TZS Bilioni 24,085,117,870** Kazi za Maendeleo) sawa na **asilimia 80** makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 60** kwa mwaka.

94. **Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo ya Jumuiya ya Kondominio kwa mwaka wa fedha 2025/2026 itaendelea kusimamia upatikanaji wa maeneo ya ujenzi wa nyumba, kufanya usajili wa Miradi ya Kondominio 16, Fleti 200 na ramani 12 Unguja na Pemba, itaendelea kuimarisha ushirikiano wa Sekta ya Nyumba Kitaifa; Kikanda na Kimataifa, itatayarisha Miongozo na kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Jumuiya za Kondominio katika maeneo ya pamoja kwa nyumba ambazo zimeshasajiliwa, itaendelea

kufanya ukaguzi na uhakiki katika Miradi ya Kondominio, itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na Usajili wa Kondominio, uundaji wa Jumuiya na Masuala ya Sekta Milki, itasimamia uandaaji wa Sheria ya Sekta Milki Nchini pamoja na kuanzisha Mfumo wa kielektroniki wa Usajili na Kuhifadhi taarifa za Kondominio.

95. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS TZS Bilioni 4,354,000,000** kutokana na Ada ya Usajili wa Kondominio.

96. **Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo ya Jumuiya ya Kondominio chini ya Idara ya Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 301,077,432,200** kwa kazi za kawaida na Maendeleo ambapo **TZS Milioni 200,832,200 Mishahara, TZS Milioni 756,600,000** kazi za kawaida na **TZS Bilioni 300,120,000,000** kwa kazi za Maendeleo.

## HN02030105 UTATUZI WA MIGOGORO KWA WAPANGAJI WA NYUMBA.

97. **Mheshimiwa Spika;** Programu ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya Utatuzi wa Migogoro kwa Wapangaji wa Nyumba inayotekelezwa na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imeanzishwa kwa Sheria ya kudhibiti kodi za

Nyumba, Sura ya 98 ya Mwaka 1953 (Cap. 98 of 1953) kwa lengo la kusikiliza na kuyatolea uamuzi mashauri yanayotokana na migogoro ya upangishaji wa Nyumba za Serikali na Nyumba binafsi. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imepokea mashauri mapya 26 (Unguja 22 na Pemba 04), hivyo kufanya Bodi hii kwa sasa kuwa na Mashauri 39 (33 Unguja na 06 Pemba). Pia, imefanikiwa kusikiliza mashauri Thelathini na mbili (32) Unguja na Pemba (Unguja 30 na Pemba 2) na imeyatolea maamuzi mashauri ya migogoro ya kodi za nyumba Kumi na Nne (14) kwa Unguja.

ii. Imetoa elimu kwa jamii kuhusu utendaji wa kazi za Bodi kwa Masheha wa Wilaya ya Mjini.

98. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba ilikadiriwa kutumia Ruzuku ya Matumizi ya Kazi za Kawaida ya **TZS Milioni 105,000,000** na **TZS Milion 78,750,000** ya Ruzuku kwa Miezi Tisa.

99. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025, fedha zilizopatikana ni Ruzuku ya Matumizi ya Kazi za Kawaida **TZS Milioni 48,390,000** sawa na **asilimia 61** ya fedha zilizopangwa kwa Miezi Tisa na asilimia **46** kwa mwaka.

100. **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma

ya utatuzi wa Migogoro ya Nyumba inayotekelezwa na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba itatoa elimu kwa Taasisi za Serikali na jamii kuhusiana na shughuli na majukumu ya kisheria ya Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Zanzibar na itaongeza ufanisi katika utoaji wa maamuzi ya kesi zinazohusiana na migogoro ya kodi za nyumba kwa kuzitolea maamuzi mashauri Thalathini (30) Unguja na Pemba.

101. **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2025/2026 naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya Kawaida **TZS Milioni 81,864,000** kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

## SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR

102. **Mheshimiwa Spika;** Shirika la Nyumba Zanzibar ni taasisi inayojitegemea iliyoanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2014. Taasisi hii imepewa Mamlaka ya kusimamia na kuendeleza Sekta ya Nyumba Zanzibar kwa kuchangia katika ukuaji wa uchumi na Maendeleo ya Makaazi kwa Wananchi wa Zanzibar ili kwenda sambamba na mahitaji ya nyumba kutokana na ongezeko la watu pamoja na utoaji wa huduma za ujenzi na ushauri elekezi. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Shirika la Nyumba imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imekamilisha ujenzi wa nyumba 72 za Makaazi na Biashara Mombasa (kwa Mchina) na nyumba zote tayari zimenunuliwa.

ii. Imekamilisha ujenzi wa Nyumba nane na Maduka 20 ya biashara Mkungu Malofa Pemba na Nyumba zote zimeuzwa na maduka yamekodishwa.

iii. Imekamilisha ujenzi wa Jengo namba 1293/94 Darajani (Kwa Fundi Abduli) na Jengo hilo tayari ameshapatiwa Muwekezaji kwa njia ukodishwaji kwa Mkataba wa muda mrefu.

iv. Imekamilisha matengenezo ya Jengo namba 1699/1705 Mkunazini (Mnadani) awamu ya kwanza na awamu ya pili inaendelea na imefikia asilimia 90 ya utekelezaji.

v. Inaendelea na ujenzi wa Jengo la Ghorofa la Makaazi na Biashara namba 2591/92 – Mchangani na limefikia asilimia 45 ya utekelezaji.

vi. Inaendelea na ujenzi wa Jengo la Makaazi na Biashara la Gorofa 5 KiembeSamaki na limefikia asilimia 35 ya utekelezaji.

vii. Inaendelea na ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Shirika la Nyumba Pemba na asilimia 40 ya utekelezaji.

viii. Imefanya ukaguzi na kutoa Mikataba 343 ya ukodishwaji kwa Wapangaji wake.

ix. Imewajengea uwezo Wafanyakazi Kumi na Tano (Unguja 14 na Pemba 1) wa fani tofauti kwa kupatiwa mafunzo ya muda mfupi kati ya hao Wanawake 4 na Wanaume 11, Wafanyakazi Kumi (Unguja 9 na

Pemba 1) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Astashahada na Shahada pamoja na kuwapatia stahiki zao Wafanyakazi Kumi na Saba (Unguja 9 na Pemba 8) ikiwemo Likizo.

x. Imeimarisha Mfumo wa kuhifadhia taarifa za wapangaji (HMS) pamoja na kuendelea ukamilishaji wa Mfumo wa **"ZHC Portal"** kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wa Shirika.

xi. Inaendelea na ujenzi wa Nyumba 3,000 Chumbuni ambapo kwa awamu ya kwanza imeanza na ujenzi wa Nyumba 1,095 zinazojengwa na Kampuni ya Zanzibar and WEIHAI kutoka China kwa njia ya Usanifu na Ujenzi (EPC+F).

**103. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/25, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Shirika la Nyumba Zanzibar ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 24,640,000,000** kutokana na vyanzo vyake mbali mbali vya mapato na Kwa Kipindi cha Miezi Tisa Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 17,191,256,500**.

**104. Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025 Shirika limefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 10,317,190,919.66** sawa na **asilimia 60.01** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 42** ya makario ya mwaka.

**105. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/25, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Shirika la Nyumba imekadiria kutumia jumla ya **TZS Bilioni**

**23,594,314,868** na **TZS Bilioni 14,326,004,476** kwa kipindi cha Miezi Tisa zilitengwa kwa ajili ya malipo ya Mishahara, Uendeshaji wa Ofisi pamoja na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambayo ni ujenzi wa nyumba mpya za makaazi na biashara na baadhi ya matengenezo ya nyumba za Shirika.

106. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025 Shirika limetumia jumla ya **TZS Bilioni 7,823,043,899.46** sawa na **asilimia 54.6** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 33.15** kwa makadirio ya matumizi yaliyopangwa kwa mwaka.

107. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Shirika la Nyumba kupitia Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi itaendelea na Miradi ya ujenzi wa nyumba 2,384 za Makaazi na Biashara katika maeneo ya mbali mbali Unguja na Pemba, Itaendelea na ujenzi wa (Awamu ya Pili) nyumba 8 za Makaazi na milango ya maduka 20 Mkungu Malofa-ChakeChake, Kuendelea kutafuta Wawekezaji kwa lengo la kushirikiana kwenye Miradi ya ujenzi wa Nyumba mpya za Makaazi na Biashara, Kuendelea kuzifanyia matengenezo Nyumba za Mji Mkongwe kwa kushirikiana na wawekezaji wenye nia ya kuekeza, Kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kwa kufanya mapitio ya mikataba ya ukodishwaji ya muda mrefu, Kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa kuwafikia Wapangaji kirahisi kwa kutumia mfumo wa simu (Mobile App) pamoja na Kuweka mazingira Bora ya kazi na kuwajengea uwezo Wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali ili kuengeza ufanisi wa kazi.

108. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu kupitia Shirika la Nyumba inatarajia kukusanya jumla ya **TZS TZS Bilioni 37,536,000,000** kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato yakiwemo makusanyo ya ndani Kodi, Mikataba, Dhamana, Tozo pamoja na kazi za Ujenzi na Ushauri Elekezi.

109. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu kupitia Shirika la Nyumba imekadiria kutumia jumla ya **TZS Bilioni 34,072,921,390**. Kati ya fedha hizo **TZS Bilioni 2,004,466,195**, Mishahara, **TZS Bilioni 1,723,790,000** Matumizi ya Kazi za Kawaida na **TZS Bilioni 30,349,665,395** kwa ajili ya Ujenzi wa Miradi na Matengenezo ya Nyumba za Shirika.

110. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Kuu **PN0203** ya Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 4,354,000,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

111. **Mheshimiwa Spika;** Ili Programu Kuu **PN0203** ya Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 301,159,296,200** ambapo **TZS Milioni 200,832,200** Mishahara, **TZS Milioni 838,464,000** Kazi za Kawaida na **TZS Bilioni 300,120,000,000** kwa Kazi za Maendeleo.

## VIPAUMBELE VYA BAJETI YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

112. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imejipanga kutekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuendelea na ujenzi wa nyumba mpya za Makaazi na Biashara pamoja na kufanya Matengenezo ya Nyumba zilizopo.

ii. Kuendelea na ujenzi wa Mifumo ya utoaji wa huduma kwa Wananchi katika Sekta ya Ardhi na Makaazi.

iii. Kuendelea na utambuzi wa Ardhi pamoja na uandaaji wa Mipango Mikuu na ya Kina ya Matumizi ya Ardhi ya Miji mbalimbali Unguja na Pemba.

iv. Kuendelea na zoezi la kliniki ya Ardhi kwa Shehia mbalimbali Unguja na Pemba ili kuwafikia Wananchi wa chini kwa kuwajengea uelewa juu ya utoaji wa huduma za ardhi, utatuzi wa migogoro ya Ardhi pamoja na masuala mengineyo yanahusiana na Sekta ya ardhi Nchini.

v. Kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya Ardhi na Makaazi kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

## MAOMBI YA IDHINI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

**113. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako litupatie idhini ya kukusanya Mapato ya Fedha **TZS Bilioni 7,614,810,000** kutoka vyanzo mbalimbali vilivyomo ndani ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi na **TZS Bilioni 10,164,108,136** kutoka vyanzo mbalimbali vilivyomo ndani Kamisheni ya Ardhi. **Kiambatanisho namba 7 (a) Kinafafanua.**

**114. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ili Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza Programu Kuu na Programu Ndogo nilizozieleza, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya **TZS Bilioni 345,485,900,000** kati ya hizo **TZS Bilioni 2,734,600,000** Mishahara, **TZS Bilioni 3,493,600,000** matumizi ya kawaida, **TZS Bilioni 3,572,700,000** Ruzuku (**TZS Milioni 507,700,000** Ruzuku ya Matumizi ya Kazi za Kawaida na **TZS Bilioni 3,065,000,000** ni Ruzuku ya Mishahara) na **TZS Bilioni 335,685,000,000** kwa kutekeleza Kazi za Maendeleo. **Kiambatanisho namba 7 (b) kinafafanua.**

**115. Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa matumizi ya Kamisheni ya Ardhi, naliomba Baraza lako kuidhinisha Matumizi ya **asilimia 50** yatokanayo na Makusanyo ya Kamisheni ya Ardhi (Retention).

## SHUKRANI

116. **Mheshimiwa Spika;** baada ya uwasilishaji huo sasa nachukua fursa hii kwa mara nyengine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia fursa, uwezo wa kuisoma Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

117. **Mheshimiwa Spika;** vilevile, naomba kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa miongozo na maelekezo yake anayotupatia iliyopelekea kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi na kutoa huduma bora kwa Wananchi kupitia Sekta ya Ardhi na Makaazi. Aidha, nawashukuru tena Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kwa maelekezo yao wanayonipatia. Wote nawaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwapa busara, uadilifu, afya njema na maisha marefu pamoja na familia zao.

118. **Mheshimiwa Spika;** kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi, Waheshimwa Wenyeviti wa Kamati za Baraza la Wawakilishi na Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa na utulivu wakati nikisoma Hotuba ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.

119. **Mheshimiwa Spika;** napenda kuwashukuru Wadau mbalimbali walioshirikiana nasi kwa njia moja au nyengine wakiwemo Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Washirika wa Maendeleo, Sekta binafsi, Asasi za Kiraia na Jamii kwa Ujumla. Wadau hao ni pamoja Wizara ya Ardhi ya Korea, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi (SJMT); Ofisi ya Rais Fedha na Mipango; Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalamu za SMZ; Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi; Wizara Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs); Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA); Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA); Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Taasisi ya Afisi ya Rais Ufuatiaji wa utendaji kazi wa Serikali (ZPDB).

120. **Mheshimiwa Spika;** vilevile, nawashukuru Shirka la Umoja wa Mataifa la Makaazi Duniani (UN – HABITAT), Benki ya Dunia, IGNFI, Kampuni ya Infinity, Zanzibar and WEIHAI, VIGAN STAN, KINGS PRIDE, HOJUNG SOLUTION ya Korea, Benki na Taasisi za Fedha; Masheha pamoja na Wananchi kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia uliochangia kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi.

121. **Mheshimiwa Spika;** Kipekee naomba niushukuru Uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi hususan Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Mheshimiwa Salha Mohammed Mwinjuma; Katibu Mkuu Ndugu Khadija

Khamis Rajab; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Mhaza Gharib Juma; Afisa Mdhamini Ndugu Bakari Ali Bakari; Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumba Ndugu Sultan Said Suleiman; Katibu Mtendaji Kamisheni ya Ardhi Ndugu Mussa Kombo Bakari; Wakurugenzi wote, Wakuu wa Taasisi na Wafanyakazi wote kwa kuwa na mimi bega kwa bega katika kuhakikisha Wizara inatekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia kulingana na Mipango Mikuu ya Kitaifa, Kikanda, Kimataifa inayohusiana na Sekta ya Ardhi na Makaazi.

122. **Mheshimiwa Spika;** Pia, Navishukuru Vyombo vyote vya habari vilivyoshirikiana nasi katika kuelimisha jamii juu ya shughuli zinazofanywa na Wizara vikiwemo ZBC TV na Redio, TBC, ZCTV, ITV, STAR TV, AZAM TV, CHANNEL 10, TIFU TV, WASAFI, Milard Ayo, Mtegani Redio, Zenj Redio, Zinjibar TV, Zanzibar Leo na Nipashe.

123. **Mheshimiwa Spika;** Vilevile, napenda kuishukuru familia yangu kwa upendo wao, michango, uvumilivu, subra na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu niliokabidhiwa. Na kwa namna ya pekee nawashukuru Kinamama wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kunipa ushirikiano mkubwa na kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali za kuwaletea Wananchi Maendeleo.

124. **Mheshimiwa Spika;** shukurani za pekee kabisa ziwaendee Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Unguja na Pemba kwa Ushirikiano wao mkubwa

walionipatia kwa kipindi chote nilichokuwa nahudumia Wizara hii. Namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie wote afya njema na maisha marefu yenye kheri ili waweze kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## HITIMISHO

**125. Mheshimiwa Spika;** nawaomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waipokee, waijadili kwa kina Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, kisha watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe makadirio haya. Tuna imani kubwa kuwa michango ya Waheshimiwa Wajumbe itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**126. Mheshimiwa Spika;** naomba kutoa hoja.



…………………………………………..

**MHESHIMIWA RAHMA KASSIM ALI (MBM)**
**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI**
**ZANZIBAR.**

# VIAMBATISHO

## KIAMBATANISHO NAMBARI: 1(a) MUHTASARI WA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA KIPINDI CHAJULAI 2024 - MACHI 2025.

| TAASISI | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA KWA MWAKA | FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOKUSANYWA JULAI 2023 – MACHI 2024 | ASILIMIA YA FEDHA ILIYOKUSANYWA (KWA MIEZI TISA) | ASILIMIA YA FEDHA ILIYOKUSANYWA (KWA MWAKA) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **AFISI KUU PEMBA** | **1422070** | Ada ya Vibali vya Ujenzi (DCU) | 36,000,000 | 27,000,000 | 15,700,000 | **58%** | **44%** |
| | **1422008** | Ada ya Mahakama | 7,000,000 | 5,250,000 | 2,458,100 | **47%** | **34%** |
| | **Jumla ndogo** | | **43,000,000** | **32,250,000** | **18,158,100** | **56%** | **42%** |
| **IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI** | **1422016** | Ada ya Vibali vya Ujenzi (DCU) | 2,127,000,000 | 1,595,250,000 | 368,671,000 | **23%** | **17%** |
| | **Jumla ndogo** | | **2,127,000,000** | **1,595,250,000** | **368,671,000** | **23%** | **17%** |
| **PROGRAM YA USIMAMIZI WA ARDHI - PN0202** | | | | | | | |
| OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI | **1422093** | Ada ya Uthamini | 500,000,000 | 375,000,000 | 152,564,759 | **41%** | **31%** |
| MAHAKAMA YA ARDHI | **1422072** | Ada ya Mahakama | 10,000,000 | 7,500,000 | 7,393,700 | **99%** | **73%** |
| | **Jumla ndogo** | | **510,000,000** | **382,500,000** | **159,958,459** | **42%** | **31%** |
| **PROGRAM YA MAENDELEO YA MAKAAZI - PN0203** | | | | | | | |
| IDARA YA MAENDELEO YA MAKAAZI | **1422119** | Ada ya Usajili wa Kondominio | 1,590,000,000 | 1,192,500,000 | 1,087,005,712 | **91%** | **68%** |
| **Jumla ndogo** | | | **1,590,000,000** | **1,192,500,000** | **1,087,005,712** | **91%** | **68%** |
| **JUMLA KUU** | | | **4,270,000,000** | **3,202,500,000** | **1,633,793,271** | **51%** | **38%** |

## KIAMBATANISHO NAMBARI 1(b) MUHTASARI WA MATUMIZI YA PROGRAMU KUU NA PROGRAMU NDOGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 – MACHI 2025 IKILINGANISHWA KWA MAKADIRIO YA MWAKA.

| PROGRAMU KUU | IDARA/ TAASISI | MAKISIO KWA MWAKA | MAKISIO KWA ROBO TATU | KILICHOPATIKANA KWA ROBO TATU | MISHAHARA NA POSHO | MATUMIZI MENGINEYO | MATUMIZI YA RUZUKU YA OC | MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO | ASILIMIA YA ROBO 3) | ASILIMIA YA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 5,836,498,000 | 4,458,053,500 | 518,858,641 | 420,528,641 | 98,330,000 | - | - | 12% | 9% |
| | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 1,821,535,000 | 1,383,871,460 | 873,525,561 | 680,872,361 | 192,653,200 | - | - | 63% | 48% |
| | Ofisi Kuu Pemba | 864,936,000 | 683,406,230 | 496,474,979 | 320,442,312 | 176,032,667 | | | 73% | 57% |
| | **Jumla ndogo** | **8,522,969,000** | **6,525,331,190** | 1,888,859,181 | **1,421,843,314** | **467,015,867** | - | - | **29%** | **22%** |
| Usimamizi wa Ardhi | Mahakama ya Ardhi | 743,799,000 | 444,774,250 | 374,153,275 | 303,603,275 | 70,550,000 | - | - | **84%** | **50%** |
| | Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali | 256,400,000 | 193,840,000 | 64,200,000 | - | | 64,200,000 | | 33% | **25%** |
| | **Jumla ndogo** | **1,000,199,000** | **638,614,250** | 438,353,275 | **303,603,275** | **70,550,000** | **64,200,000** | - | **69%** | **44%** |
| | Kamisheni ya Ardhi | 3,003,300,000 | 2,252,475,000 | 2,270,555,233 | 2,270,555,233 | - | - | - | 101% | 76% |
| | **Jumla ndogo** | **3,003,300,000** | **2,252,475,000** | 2,270,555,233 | **2,270,555,233** | - | - | - | **101%** | **76%** |
| Maendeleo ya Makaazi | Idara ya Maendeleo ya Makaazi | 40,431,432,000 | 30,346,039,000 | 24,300,717,380 | 128,818,710 | 86,780,800 | | 24,085,117,870 | 80% | 60% |
| | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba | 105,000,000 | 78,750,000 | 48,390,000 | - | - | 48,390,000 | - | 61% | 46% |
| | **Jumla ndogo** | **40,536,432,000** | **30,424,789,000** | **24,349,107,380** | **128,818,710** | **86,780,800** | **48,390,000** | **24,085,117,870** | **80%** | **60%** |
| | **JUMLA KUU** | **53,062,900,000** | **39,841,209,440** | **28,946,875,069** | **4,124,820,532** | **624,346,667** | **112,590,000** | **24,085,117,870** | **73%** | **55%** |

## KIAMBATANISHO NAMBARI 2

## MAENEO YALIYOFANYIWA UKAGUZI WA UJENZI NA KAMATI YA USIMAMIZI NA UDHIBITI UJENZI

| SN | WILAYA | ENEO |
|---|---|---|
| 1. | Wilaya ya Kati | Dunga, Uroa, Chwaka, Tunguu na Jumbi |
| 2. | Wilaya ya Kusini | Michamvi, Kizimkazi, Bwejuu na Paje |
| 3. | Wilaya ya Mjini | Mwembemakumbi, Miembeni, Jang'ombe, Kikwajuni Juu, Sebleni, Meya, Saateni, Urusi, Chumbuni, Masumbani, Kilimani, Kijangwani, Magomeni na Mkele |
| 4. | Wilaya ya Magharib A | Mbuzini, Kijichi, Mwera, Kianga, Kikaangoni, Mwembemchomeke, Mkanyageni, Mfenesini na Chuini |
| 5. | Wilaya ya Magharib B | Kwarara, Kiembesamaki, Uwandani, Nyamanzi, Shakani, Chukwani, Mbweni, Bweleo, Buyu, Kibondeni, Jumbi, Sokoni, Kisauni, Kisakasaka, Kombeni, Migombani, Mambosasa, Kipungani, Mnarani, Mitondooni, Dimani na Maungani |
| 6. | Wilaya ya Kaskani A | Nungwi, Fukuchani, Kendwa Mto wa Pwani, Mkokotoni, Kinyasini, Kidoti, Tazari, Matemwe na Banda Kuu na Pwani Mchangani. |
| 7. | Wilaya ya Kaskazini B | Kiwengwa, Kazole na Mangapwani |
| 8. | Kusini Pemba | Chakechake na Mkoani |
| 9. | Kaskazini Pemba | Michweni |

## KIAMBATANISHO NAMBARI 3

## IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOPATIWA LIKIZO NA STAHIKI

| NAM. | AINA YA STAHIKI | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | **WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI- UNGUJA** | | | |
| 1. | LIKIZO | 6 | 8 | 14 |
| 2. | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | 3 | - | 3 |
| 3. | WALIOAJIRIWA | 2 | 1 | 3 |
| 4. | UBANI | - | 1 | 1 |
| 5. | PERFORMANCE APPRISAL | 42 | 48 | 90 |
| | **JUMLA** | **53** | **58** | **111** |
| | **KAMISHENI YA ARDHI** | | | |
| | LIKIZO | 13 | 15 | 28 |
| | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | 272 | 196 | 468 |
| | WALIOAJIRIWA | - | - | - |
| | UBANI | 2 | 1 | 3 |
| | PERFORMANCE APPRISAL | - | - | - |
| | **JUMLA** | **287** | **212** | **499** |
| | **MAHKAMA YA ARDHI** | | | |
| | LIKIZO | 1 | - | 1 |
| | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | 9 | - | 9 |
| | WALIOAJIRIWA | - | - | - |
| | UBANI | 2 | 1 | 3 |
| | PERFORMANCE APPRISAL | - | - | - |
| | **JUMLA** | **12** | **1** | **13** |
| | **MTHAMINI MKUU WA SERIKALI** | | | |
| | LIKIZO | 3 | 6 | 9 |
| | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | - | - | - |
| | WALIOAJIRIWA | - | - | - |
| | UBANI | 2 | - | 2 |
| | PERFORMANCE APPRISAL | - | - | - |
| | **JUMLA** | **5** | **6** | **11** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **SHIRIKA LA NYUMBA** | | | |
| | LIKIZO | 27 | 15 | 42 |
| | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | 1 | 2 | 3 |
| | WALIOAJIRIWA | 1 | 1 | 2 |
| | UBANI | - | 1 | 1 |
| | PERFORMANCE APPRISAL | - | - | - |
| | **JUMLA** | **29** | **19** | **48** |
| | **AFISI KUU-PEMBA** | | | |
| | LIKIZO | 6 | 4 | 10 |
| | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | 4 | 4 | 8 |
| | WALIOAJIRIWA | - | - | - |
| | UBANI | - | - | |
| | PERFORMANCE APPRISAL | 9 | 8 | 17 |
| | **JUMLA** | **19** | **16** | **35** |

## KIAMBATANISHO NAMBARI: 4(a)

## MAFUNZO YA MUDA MFUPI KWA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

| S/N | TAASISI | M'ME | | W'KE | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | NDANI YA NCHI | NJE YA NCHI | NDANI YA NCHI | NJE YA NCHI | |
| 1 | UTUMISHI NA UENDESHAJI | 16 | - | 18 | - | **34** |
| 2 | MIPANGO SERA NA UTAFITI | 1 | | 1 | | **2** |
| 3 | IDARA YA MAENDELEO YA MAKAAZI | 1 | - | - | - | **1** |
| 4 | MAHAKAMA YA ARDHI | | | 1 | | 1 |
| 5 | SHIRIKA LA NYUMBA | 18 | - | 12 | - | 30 |
| 6 | MTHAMINI MKUU | - | - | - | - | **0** |
| 7 | KAMISHENI YA ARDHI | 12 | | 15 | | **27** |
| | **JUMLA KUU** | **48** | | **47** | - | **95** |

## KIAMBATANISHO NAMBARI: 4(b)

## MAFUNZO YA MUDA MREFU KWA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI 2024/2025

| TAASISI | AINA YA MAFUNZO | W'ME | W'KE | JUMLA | CHUO | MWAKA WA KUMALIZA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI** | Degree in Mass Communication | | 1 | 1 | Open University-Zanzibar | 2025 |
| | Masters in Software Engineering | 1 | | 1 | University of Nankai (CHINA) | 2025 |
| **MAHKAMA YA ARDHI** | Degree in Law and Sharia | | 3 | 3 | Zanzibar University(ZU) | 2025 |
| | Master in Human Resource Management | | 1 | 1 | Tanzania Institute of Accountancy (TIA) | 2026 |
| **SHIRIKA LA NYUMBA** | Masters in Human Resource Management with Information | | 1 | 1 | Tanzania Institute of Accountancy (TIA) | 2026 |
| | Bachelor Degree in Procurement & Supply | | 1 | 1 | Open University (Out)Zanzibar | 2026 |
| | Masters in Science In Economic and Finance | 1 | | 1 | Zanzibar University (ZU) Niversity | 2025 |
| | Masters in Bussiness Administration | | 1 | 1 | Zanzibar University (ZU) Niversity | 2026 |
| | Bachelor Degree in Record and Archives | | 1 | 1 | Utawala Wa Umma (IPA) | 2027 |
| | Masters in International Business | 1 | | 1 | Harbin University of Commerce-China | 2026 |
| | Master’s in Business Administration In a Corporate | 1 | | 1 | Tanzania Institute of Accountancy (TIA) | 2026 |
| | Masters in Project Management | 1 | | 1 | Open University-Zanzibar | 2025 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Master in Economics and Finance in Project | | 1 | 1 | Zanzibar University(ZU) | 2026 |
| | Bachelor Degree In Architecture | | 1 | 1 | Ardhi University-Dar-Es-Salaam | 2028 |
| | Diploma in Business Admiration | | 1 | 1 | Institute Of Professional And Innovational Development-Pemba | 2025 |
| **KAMISHENI YA ARDHI** | Phd in Science in Architecture | 1 | | 1 | Aalto University - Ufini-Finland | 2025 |
| | Degree in Secretarial Information Management | | 1 | 1 | Kampla Unirvesity-Uganda | 2028 |
| | Masters in Technical In Data Science & Artificial Intelligence | 1 | | 1 | Indian Institute Of Technology Madras-Bweleo Zanzibar | 2025 |
| | Masters In Comparative Laws | 1 | | 1 | Zanzibar University(Zu) | 2025 |
| | Degree in Civil Engener | | 1 | 1 | Karume Technology Institute | 2025 |
| | Degree in Management In Social Development | | 1 | 1 | Mwalimu Nyerere Memorial Academy | 2025 |
| | Degree in Secretarial Information and Office Management | | 1 | 1 | Kampala University | 2026 |
| | Degree in Information communication and Technology | 1 | | 1 | SUZA | 2025 |
| | Diploma in Computer Science & It, Network | 1 | | 1 | Kampala University-Uganda | 2026 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Bachelor Degree In Science in Real Estate Finance and Investment | 1 | | 1 | Ardhi University-Dar-Es-Salaam | 2027 |
| | Masters in Hydrographic Survey | 1 | | 1 | University Of Technology Malaysia | 2026 |
| | Masters Program Of Urban And Rural Planning | 1 | | 1 | Beijing Jiaotong University-China | 2026 |
| | Degree in Project Planning and Management | 1 | | 1 | "Institute Of Counting And Professional Studies" Chukwani | 2026 |
| **OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI** | Degree in Law and Sharia | 1 | | 1 | Chuo Kikuu Huria (Out-Zanzibar) | 2027 |
| | Degree in Record and Achieves Management | | 1 | 1 | Chuo Cha Utawala Wa Umma (IPA) | 2027 |
| | Diploma in Human Resource Management | | 1 | 1 | Chuo Cha Utawala Wa Umma(IPA) | 2026 |
| **OFISI KUU - PEMBA** | Degree in record and Achieve Management | | 1 | 1 | Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) | 2026 |
| | Degree Procurement and Logistic Management | 1 | | 1 | Tanzania Institute Of Accountancy (TIA) | 2025 |
| | Degree in Secretarial Information Management | | 1 | 1 | Kampla Unirvesity-Uganda | 2026 |
| | Diploma in Law | 1 | | 1 | Zanzibar University(ZU) | 2026 |

## KIAMBATANISHO NAMBARI: 5

## KESI ZILIZOPOKELEWA NA KUTOLEWA MAAMUZI KWA KIPINDI CHA KUTOKA JULAI, 2024 HADI MACHI 2025.

| MKOA HUSIKA | | KESI MPYA ZILIZOFUNGULIWA | KESI ZILIZOTOLEWA MAAMUZI | KESI ZINAZOOENDELEA MAHAKAMANI |
|---|---|---|---|---|
| UNGUJA | Mjini Magharibi | 59 | 51 | 97 |
| | Kaskazini Unguja | 29 | 19 | 38 |
| | Kusini Unguja | 28 | 16 | 52 |
| PEMBA | Kaskazini Pemba | 20 | 13 | 24 |
| | Kusini Pemba | 34 | 41 | 32 |
| **JUMLA KUU** | | **170** | **140** | **243** |

## KIAMBATANISHO NAMBARI: 6
## USAJILI NA UKAGUZI WA MIRADI YA KONDOMINIO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

| NAMB. | JINA LA MRADI | WILAYA | MAHALI ULIPO |
|---|---|---|---|
| 1. | Said Majid Said (Zahran Abdalla Salum and Seif Said Hemed As Developer) | MJINI | VIKOKOTONI |
| 2. | Zantexas Investment limited | MAGHARIBI ‘B’ | BWELEO |
| 3. | Abdulkarim Mohammed Abdi and Tofa Saleh Suleiman | MAGHARIBI ‘B’ | MWANAKWEREKWE |
| 4. | Ballardini Company Limited (Ycona Luxury Resort) | KATI | UROA |
| 5. | Frog Traveler Limited | KASKAZINI ‘A’ | NUNGWI |
| 6. | Vigor International Company Limited (Johari as Developer) | KASKAZINI ‘A’ | NUNGWI |
| 7. | Moyo Mzuri Villas Resort Zanzibar Limited | KASKAZINI ‘A’ | FUKUCHANI |
| 8. | Just Heaven Company Limited | KASKAZINI ‘A’ | MATEMWE |
| 9. | Itaset Company limited | KASKAZINI ‘B’ | KIWENGWA |
| 10. | Sea View Property Limited (Lapili Residence),(Breeze Residence), AND (Padel Sporting& Residence) | KASKAZINI ‘B’ | KIWENGWA |
| 11. | AD Astra Development Limited | KUSINI | PAJE |
| 12. | Mussa Dream Houses | KUSINI | PAJE |
| 13. | Safari Njema Group Limited | KUSINI | PAJE |
| 14. | Zanzibar Villas Limited | KUSINI | PAJE |
| 15. | Sam 2009 Limited | KUSINI | MAKUNDUCHI |
| 16. | Floton Africa Company limited | KUSINI | PAJE |
| 17. | Jambiani Group Company Limited | KUSINI | JAMBIANI |
| 18. | Nyumba za Maendeleo | WETE | MTEMANI |
| 19. | Dimbani Villas & Property Management Company Limited | KUSINI | KIZIMKAZI |
| 20. | Johari Developers Limited | KUSINI | KIZIMKAZI |

## KIAMBATANISHO NAMBARI: 7(a)
## MAKADIRIO YA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA FUNGU LA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

| TAASISI | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA |
|---|---|---|---|
| **PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI - PN0201** | | | |
| OFISI KUU PEMBA | 1422016 | Ada ya Vibali vya Ujenzi (DCU) | 80,800,000 |
| | 1422119 | Ada ya usajili wa Kondominio | 20,000,000 |
| | 1422070 | Fii ya Korti | 15,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **115,800,000** |
| IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI | 1422016 | Ada ya Vibali vya Ujenzi (DCU) | 2,610,010,427 |
| | **Jumla ndogo** | | **2,610,010,427** |
| **JUMLA** | | | **2,725,810,427** |
| **PROGRAMU YA USIMAMIZI WA ARDHI -PN0202** | | | |
| MTHAMINI WA ARDHI | 1422093 | Ada ya Uthamini | 520,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **520,000,000** |
| MAHAKAMA YA ARDHI | 1422070 | Fii ya Korti | 15,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **15,000,000** |
| KAMISHENI YA ARDHI | **1422093** | Ada ya Uthamini | 135,526,049 |
| | **1422028** | Muongozo wa Matumizi ya Ardhi | 450,893,124 |
| | **1422008** | Nyaraka za Ardhi | 1,415,307,241 |
| | **1422043** | Ada ya Upimaji na Ramani | 1,574,240,104 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **1422072** | Ada ya Usajili wa Ardhi | 130,951,110 |
| | **1422090** | Uhalishaji wa Ardhi | 6,457,190,512 |
| | **Jumla ndogo** | | **10,164,108,140** |
| **JUMLA** | | | **10,699,108,140** |
| **PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKAAZI – PN0203** | | | |
| IDARA YA MAENDELEO YA MAKAAZI | 1422119 | Ada ya usajili wa Kondominio | 4,354,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **4,354,000,000** |
| **JUMLA KUU** | | | **17,778,918,567** |

## KIAMBATANISHO NAMBARI: 7 (b)
## MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI KWA FUNGU LA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

| Na. | PROGRAMU | PROGRAMU NDOGO | TAASISI/IDARA | MAKISIO KWA MWAKA 25/26 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **MATUMIZI MENGINEYO** | **MISHAHARA** | **RUZUKU** | **KAZI ZA MEANDELEO** | **JUMLA YA FEDHA ILIYOPANGWA** |
| 1 | Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 1. Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 803,400,000 | 260,795,200 | – | 35,565,000,000 | **36,629,195,200** |
| | | 2. Utawala na Uendeshaji | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | **612,410,000** | **1,440,835,200** | – | – | **2,053,245,200** |
| | | 3. Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | Afisi Kuu Pemba | 839,326,000 | 444,138,200 | – | – | **1,283,464,200** |
| | | Jumla ndogo | | 2,255,136,000 | 2,145,768,600 | – | **35,565,000,000** | |
| 2 | Usimamizi wa Ardhi | 1. Usimamizi wa Ardhi | Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali | – | – | 507,700,000 | – | **507,700,000** |
| | | | Mahakama ya Ardhi | 400,000,000 | 387,999,200 | – | – | **787,999,200** |
| | | | Kamisheni ya Ardhi | – | 3,065,000,000 | – | – | **3,065,000,000** |
| | | **Jumla Ndogo** | | **400,000,000** | **3,452,999,200** | **507,700,000** | **-** | |
| 3 | Maendeleo ya Makaazi | 1. Maendeleo ya Makaazi | Idara ya Maendeleo ya Makaazi | 756,600,000 | 200,832,200 | – | 300,120,000,000 | **301,077,432,200** |
| | | | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba | 81,864,000 | – | – | – | **81,864,000** |
| | | | **Jumla ndogo** | **838,464,000** | **200,832,200** | – | **300,120,000,000** | **301,159,296,200** |
| | | | **JUMLA KUU** | **3,493,600,000** | **5,799,600,000** | **507,700,000** | **335,685,000,000** | **345,485,900,000** |